



SERA YA HAKI ZA BINADAMU

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) imedhamiria kuheshimu Haki za Binadamu pamoja na sheria zinazotumika katika shughuli zetu zote na kutekeleza Kanuni za Mwongozo za Umoja wa Mataifa kuhusu kazi na Haki za Binadamu (United Nations Guiding Principles on Business and Human Rights 'UNGPs'), Kanuni za Umoja wa Mataifa za Maafikiano juu ya maswala ya kidunia, Miongozo ya OECD kwa ajili ya Mashirika ya Kimataifa, mikataba ya msingi ya Shirika la Kazi duniani na Kanuni za Hiari zinazohusu Ulinzi na Haki za Binadamu.

Sera hii ya Haki za Binadamu inalenga kufafanua dhamira ya EACOP kwa Haki za Binadamu kwa manufaa ya wadau wote wa ndani na nje.

DHAMIRA YA EACOP KATIKA SHUGHULI ZETU ZOTE NI:

- Kuheshimu haki za binadamu katika utekelezaji wa shughuli zetu za kibiashara.
- Kuhakiki uzingativu endelevu wa Haki za Binadamu kwa kutumia mbinu ya ubainishaji wa hatari, kutambua, kutathimini, kutenda, kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu hatari za Haki za Binadamu na athari zinazohusiana na shughuli za EACOP, ikiwa ni pamoja na kuheshimu haki za watu walio katika mazingira hatarishi na vikundi vinyavyobainishwa kama wazawa kulingana na viwango vya kimataifa, ikimaanisha Wa-masai, Wa-akie, Wa-barbaig na Wa-taturu.
- Kuheshimu jinsia na kuhakikisha uwakilishi, ushiriki na maendeleo ya wanawake katika kutekeleza shughuli zetu.
- Kudumisha mchakato thabiti wa ushirikishwaji wa wadau ikiwa ni pamoja na kupeana taarifa, mashauriano yenye tija na jumuishi pamoja na mazungumzo na wadau ambaao wanaweza kueleza madukuduku yao kwa uwazi.
- Kushiriki katika mashauriano mahususi na jumuiya za wenyeji zilizoguswa moja kwa moja na shughuli zetu kwa njia ambayo ni sahihi kitamaduni, kwa wakati unaofaa na kwa heshima na kujumuisha madukuduku ya wadau na kuyatolea mrejesho pale inapofaa.
- Kutoa fursa ya kupata suluhisho kwa wadau walio-athirika kuititia utekelezaji wa taratibu za malalamiko zinazowiana na vigezo vya ufanisi vya UNGP. Kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi na mishahara kwa wafanyakazi wa EACOP inaheshimu utu wa binadamu na kuwataka wakandarasi wakubwa na

wadogo na hata watoa huduma wetu wanafanye vivyo hivyo. Hii ni pamoja na kuwa na mazingira ya kazi yanayozingatia afya na usalama kazini ambapo wafanyakazi wanalinidwa dhidi ya ajali, majeraha na magonjwa yatokanayo na kazi husika.

- Kukataza:
 - Ubaguzi unaozingatia asili au mahali atokako mtu, jinsia, umri, ulemavu, utambulisho wa jinsia au tabia zinazohusiana na haya.
 - Aina yoyote ya unyanyasajji.
 - Kazi ya kulazimishwa au lazima.
 - Ajira kwa Watoto.
- Kuheshimu haki ya uhuru wa kutoa maoni, kujieleza, kupata taarifa, ushirika, majadiliano ya pamoja, uhuru wa mawazo, dhamiri, na dini.
- Kukuza Kanuni za Hiari za Ulinzi na Haki za Binadamu wakati wa ushirikishwaji wa vikosi vyovyothe vya ulinzi vya umma na kuzitekeleza wakati wa kukiutmia watoa huduma binafsi za ulinzi.
- Kueleza kwa serikali wenyeji na washikadau wengine kuhusu dhamira yetu ya kuheshimu haki za binadamu. Pale ambapo kuna tofauti kati ya hitaji la kisheria na sera hii ya haki za binadamu, katika mazingira haya, kadri inavyowezekana tutaheshimu kanuni za haki za binadamu zinazotambulika kimataifa kwa kiwango kikubwa.
- Utekelezaji wa sera hii utapitiwa mara kwa mara na kamati madhubuti na kuboreshwa kulingana na dhamira yetu ya uboreshaji endelevu.

Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa EACOP. Tunawahimiza washirika wetu na wakandarasi kutenda kwa namna inayolingana na kanuni zilizowekwa katika sera hii. Tunakuza kikamilifu ufahamu wa Haki za nadamu na heshima pamoja na washirika wetu, ikiwa ni pamoja na kupokea na kujumuisha mifumo sahihi ya kisheria na kimikataba, mafunzo na ukuzaji wa hatua za mwingiliano wa kisekta pale inapofaa. sahihi ya kisheria na kimikataba, mafunzo na ukuzaji wa hatua za mwingiliano wa kisekta pale inapofaa.